

**HOTUBA YA MHESHIMIWA ZELOTE STEPHEN ZELOTE
MKUU WA MKOA WA RUKWA KATIKA UZINDUZI WA
BODI YA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA
MAZINGIRA SUMBAWANGA TAREHE 17 AGOSTI, 2016**

Ndugu Mwenyekiti wa Bodi,

Ndugu Wajumbe wa Bodi,

Ndugu Wafanyakazi wa SUWASA.

Nashukuru sana kwa kupata heshima ya kuwa Mgeni Rasmi katika uzinduzi wa Bodi mpya ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Sumbawanga.

Napenda kukupongeza Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Bodi kwa kuteuliwa kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia Julai 2016 hadi Juni 2019 kuwa wajumbe wa Bodi hii muhimu ambayo itasimamia Mamlaka katika kutoa huduma nzuri ya Majisafi na Uondoaji wa Majitaka katika Manispaa yetu ya Sumbawanga. Pia ninapenda kuwashukuru sana wajumbe wa Bodi iliyomaliza muda wake mwezi Juni 2016. kwa kazi nzuri iliyofanyika katika kipindi chake cha miaka mitatu iliyopita.

Ndugu Mwenyekiti,

Hali ya Huduma ya Majisafi na Uondoaji wa Majitaka katika mji wetu wa Sumbawanga imekuwa haitoshelezi kwa kipindi kirefu. Mji hukabiliwa na uhaba wa maji kila mwaka hasa wakati wa kiangazi. Upanuzi wa miundombinu ya maji hauendi sambamba na ukuaji wa mji wa Sumbawanga ambao unapanuka haraka kutokana na ongezeko la watu, shughuli za kiuchumi na maendeleo ya sekta nyingine kama vile barabara, mawasiliano, elimu, biashara nk. Pengo kati ya mahitaji ya maji na kiasi cha maji kinachopatikana ni kubwa, wastani wa asilimia 35 kiangazi hadi asilimia 60 masika. Hali hii ni kero kwa wananchi na inachelewesha kuongeza maendeleo ya sekta nyingine zinazotumia maji kama viwanda, mahoteli nk

Mji wa Sumbawanga hauna mfumo rasmi wa kuondoa majitaka katika nyumba za watu. Huduma ya majitaka ilikuwa inatolewa na Manispaa ya Sumbawanga kwa kutumia gari la mwaka 1990 ambalo limechakaa na miaka ya hivi karibuni gari la mtu binafsi limekuwa likitumika pia. Nashukuru kusikia kuwa huduma ya uondoaji majitaka imenza kutolewa na SUWASA katika Manispaa yetu tangu 01 Julai, 2016.

Ndugu Mwenyekiti,

Pamoja na mapungufu niliyoyataja, wafanyakazi wa Mamlaka wamefanya kazi kubwa ya kutoa huduma ya maji mjini Sumbawanga katika mazingira magumu hasa wakati wa kiangazi. Ninajua zipo changamoto nyingi zilizo nje ya uwezo wa Mamlaka ikiwa ni pamoja na kukauka kwa vyanzo vya maji, uchakavu wa miundombinu ya maji, wizi wa maji, uhaba wa watumishi wenye sifa nk. Pamoja na changamoto hizi, Mamlaka imeendelea kupiga hatua kila mwaka katika kuboresha huduma na kukusanya mapato hadi kufikia hatua ya kuweza kujitegemea kwa gharama zote za uendeshaji ikiwa ni pamoja na mishahara ya wafanyakazi **44** tangu mwezi Oktoba 2007.

Mamlaka imekuwa inapata hati safi kila mwaka hali inayoashiria uadilifu katika matumizi ya Rasilimali za Umma. Ninawapongeza wafanyakazi wote wa Mamlaka na ninawataka waendeleo na juhudi hizi nzuri.

Ndugu Mwenyekiti,

Nimepata faraja kusikia kuwa Mamlaka inaendelea na ujenzi wa mradi wa kuboresha huduma ya maji na Usafi wa Mazingira katika mji wa Sumbawanga kwa msaada wa **Sh.Bilioni 31** kutoka Umoja wa Ulaya na Serikali ya Ujerumani

tangu mwezi Machi 2013. Hadi mwezi Juni 2016 utekelezaji wa mradi umefikia asilimia **85**.

Ninapenda kuwashukuru sana wahisani wa Umoja wa Ulaya na Serikali ya Ujerumani kwa msaada wa kugharamia ujenzi wa mradi huo wa maji. Ninatoa wito kwa wale wote wanaohusika katika mradi huu, yaani Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Bodi ya SUWASA, Mkandarasi, Mtaalamu Mwelekezi na Mamlaka, wafanye kazi kwa bidii ili kazi zilizobakia ziweze kukamilika kwa ubora unaotakiwa na bila kuwepo ongezeko la gharama ili wakaazi wa Manispaa ya Sumbawanga waanze kupata huduma iliyokusudiwa.

Ndugu Mwenyekiti,

Ninapenda Bodi mpya na Menejimenti ya Mamlaka kuzingatia mambo yafuatayo:-

- (i) Juhudi ziendeele za kuutunza mradi wa maji uliopo sambamba na kukamilisha mradi mpya unaoendelea kujengwa. Juhudi hizo ni pamoja na kuifanyia matengenezo miundombinu ya maji mara kwa mara ili iendeele kufanya kazi vizuri na kumhimiza Mkandarasi akamilishe kazi zilizobakia.

- (ii) Mamlaka itunze vyanzo vyake vya maji, visima na mito ili visikauke. Utunzaji wa vyanzo vya maji uendelee kufanyika kwa kuwashirikisha wananchi wanaoishi karibu na vyanzo vya maji, Taasisi mbali mbali, wadau wa mazingira na wananchi kwa ujumla.
- (iii) Mamlaka iweke nguvu ya kutosha katika kukusanya mapato yake ili iendelee kupiga hatua katika kujitegemea na kufanya shughuli za maendeleo, ikiwa ni pamoja na kufuatilia madeni ya Taasisi za Serikali.
- (iv) Uzoefu unaonyesha miradi mipya ya maji ikianza kufanya kazi, wingi wa maji yasiyolipiwa unaongezeka. Mamlaka ijitahidi kupunguza wingi wa maji yasiyolipiwa sasa, na baadaye miradi mipya itakapokamilika.
- (v) Mradi mpya utakapokamilika utakuwa na changamoto za uendeshaji ikiwa ni pamoja na bili kubwa za umeme na matengenezo ya pampu za umeme 17 zitakapoongezeka ukilinganisha na pampu nne zilizopo sasa. Mamlaka iandae wataalamu wa kuendesha mitambo hiyo ya umeme na kubuni njia za kuongeza mapato ili kuweza kulipa bili za umeme. Ikiwa ni

pamoja na kuomba EWURA kurekebisha bei za maji za sasa.

- (vi) Wananchi waelimishwe kuhusu maamuzi ya Bodi yanayowahusu. Vifanyike vikao vya wadau mara kwa mara ili wananchi wapate fursa ya kutoa maoni yao na kupatiwa majibu.
- (vii) Mamlaka ifuatilie kwa karibu utendaji kazi wa wafanyakazi wake. Wafanyakazi wajikite katika kuondoa kero za wateja, utaratibu wa kufanya kazi kwa mazoea uachwe mara moja. Wafanyakazi watakaothibitika kuwa ni wala rushwa, wazembe au kukosa uaminifu, wachukuliwe hatua mara moja.
- (viii) SUWASA kwa kushirikiana na Manispaa na Taasisi zingine ikamilishe zoezi la kupata Hati Miliki za viwanja na maeneo yenye miundombinu ya maji.
- (ix) Ninatoa wito kwa wateja wote wa Mamlaka walipe bili zao za maji kwa wakati ili Mamlaka iwe na uwezo wa kuendelea kujiendesha. Inatakiwa kuwa na makusanyo ya kutosha ili kuweza kulipa gharama za uendeshaji

kwa wakati ili SUWASA iendelee kutoa huduma bora na endelevu.

Ndugu Mwenyekiti,

Napenda kumalizia kwa kuitakia Bodi Mpya mafanikio makubwa katika kipindi cha miaka mitatu itakapokuwa madarakani. Ofisi yangu inawaahidi ushirikiano muda wote kadri itakavyowezezana.

Mwisho napenda kutangaza ***BODI YA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MANISPAA YA SUMBAWANGA IMEZINDULIWA RASMI.***

Zelote Stephen Zelote
**MKUU WA MKOA
RUKWA**

**RATIBA YA UZINDUZI WA BODI MPYA YA MAMLAKA
YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA
SUMBAWANGA TAREHE 17/08/2016.**

MUDA	TUKIO	MHUSIKA
3.30	Wajumbe wa Bodi na wafanyakazi kuingia ukumbi wa SUWASA	MD-SUWASA
4.00	Mgeni Rasmi kuingia ukumbini	Mgeni Rasmi/ MD – SUWASA
4.05	Utambulisho	MD SUWASA
4.10	Taarifa ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Sumbawanga	MD-SUWASA
4.15	Neno kutoka kwa Mkurugenzi Mstaafu	MD - Mstaafu
4.20	Neno kutoka kwa Mwenyekiti wa Bodi na baadaye kumkaribisha Mgeni Rasmi, kutoa vyeti kwa Bodi ya zamani.	Mwenyekiti wa Bodi
4.30	Hotuba ya Uzinduzi wa Bodi	Mgeni Rasmi
4.50	Mgeni Rasmi kuondoka	MD-SUWASA
5.00	Kuendelea na kikao cha Bodi	MD-SUWASA